SERA YA UTAWALA
Maudhui ya Mtaala wa Kidini na Shughuli katika Shule za Umma
CUR-A002

Sera zinapitiwa mara kwa mara. Kwa toleo la hivi karibuni tafadhali tembelea, https://salkeiz.sharepoint.com/qam/SitePages/Home.aspx

1. Shule za Umma za Salem-Keizer inaamini kuwa wanafunzi wote wanastahili kupata na kujumuishwa kwa pamoja, kwenye usalama na ukaribisho mashuleni. Tunatambua kuwa mtazamo wa maoni kuhusiana na uhusiano wa shule na kidini ni tofauti. Maoni ya jamii ni muhimu kwenye kuweka sera. Wilaya hata hivyo, lazima itoe uzito wa msingi kwenye Katiba ya Amerika na Jimbo la Oregon, sheria za serikali, na maamuzi yaliyofanywa kwa mahakama husika wakati wa kuweka miongozo ya kufanya maamuzi kuhusu dini na shughuli za kuhusiana na ufanyaji wake. Kifungu za Kuanzishwa ndani ya Muswada wa Haki unakataza chombo cha serikali, kujumuisha shule za umma, kutengeneza sheria yoyote au kanuni inayowapendelea dini moja au hakuna dini. Haki ya kutenda kwa dini au hakuna dini kabisa ni miongoni wa misingi zaidi ya uhuru inayodhaminiwa na Muswada wa Haki.

Maongezi ya Mwanafunzi

2. Mwanafunzi anahaki ya kuongelea mada za kidini, kama kulingana na mada za siasa (INS-A029).

   2.1. Mwanafunzi anayepata unyanyasaji kwa matokeo ya kutumia haki yao kuongea kuhusu mada za kidini anaweza kutoa taarifa hii kwa msimamizi wa shule au mfanyakazi mwingine wa shule

   2.2. Maongezi ya dini ambayo yanaleta unyanyasaji kwa kulenga mtu binafsi au kundi la watu hayalindwi chini ya sera ya maongezi

      2.2.1. Unyanyasaji unaelezewa kwenye INS-M001 kama “ni kitendo chochote ambacho kinaingiliana kwa kikubwa na fursa ya elimu ya mtu au uwezo, na unatokea katika mazingira ya shule, na pia shughuli zilizozaminiwa na shule, na usafiri kutolewa na shule au kwenye kituo chochote cha basi la shule; na hiyo ina madhara kwa kumuweka mtu kuwa na hofu ya kuumizwa au kuwa na wasiwasi wa kuharibiwa maeneo yake; au kujenga mazingira ya uhasama ya kielimu ambayo yanatumika kutishia, kudhalilisha, kuudhi au kutesa mtu mwingine.”

Ufundishaji

3. Mafundisho yanayo jumuisha maudhui ya dini na/au nyezo kwa kutumia dini yatafanyika kwa lengo la kutokuwa na upande wowote, siyo ya ibada[1] namna na atatumikia watu wa ulimwengu[2] kwa makusudi ya elimu.

   3.1. Nyezo za ufundishaji lazima kuchaguliwa kupitia vigezo vilivyowekwa kwenye sera za CUR-A001, CUR-P001 na CUR-P003

   3.2. Masomo ya kijamii,fasihi, sanaa na mengine nidhamu ya ufundishwaji kwenye shule inaweza kujumuisha mwelekeo wa dini.

      3.2.1. Mafunzo ya haya kujumuisha mwelekeo wa dini, hayatatakiwa kuchagua au kupendelea na kuipa uzito dini moja, au dini kwa ujumla, au hakuna dini na hakuna kutambulisha dini au kutumia kama sehemu ya ibada.

      3.2.2.. Matumizi ya kutumia ishara kama sehemu ya kusoma inaruhusiwa kama zinatumika kama ishara ya urithi wa dini au nyenzo za ufundishaji.

[1] Siyo ya ibada maana yake ni mazungumzo au vitendo vinavyoelezea au utelekezaji wa imani binafsi

[2] Njia za kidunia maana yake ni mitazamo, vitendo au maongezi ambayo hayana msingi wa kidini

3.2.2.1. Hizi alama zinaweza kuonyeshwa kama mtitiriko kulingana na ramani ya kiwango kwa wilaya.

3.2.2.2. Maonyesho yanatumika kama msingi wa kufundishia au nyenzo na kuwa na muda maalumu na siyo kupitiliza kwenye mafunzo au kitengo cha masomo

3.3. Vigezo vinavyotumika kwenye mwongozo wa uchunguzi wa elimu kwenye masomo ya dini kutoegemea upande wowote,kwa usawa na ufanisi wa elimu unaotarajiwa kwenye maeneo yote ya mtaala.

3.4. Nyenzo na shughuli zinapaswa kuwa nyeti kwa jamii ya Amerika yenye tamaduni nyingi na lazima ielimishe badala ya kufundisha.

3.5. Wanafunzi hawata zuiliwa kwenye kuelezea imani ya dini au mawazo yao kwenye kazi ya darasani, kujumuisha utunzi, kuandika, muziki, sanaa, mabishano, majadiliano darasani, tathmini au mitihani, ambapo inahusika na inafaa kwenye kazi ya shule.

4. Nyenzo zote za kufundishia kujumuisha mwelekeo wa kidini, kujumuisha muziki, sanaa, fasihi, vyanzo vya kihistoria, na/au shughuli lazima kuhusiana na malengo ya mwafunzi kwenye kujifunza ya kidunia au ya kiwango.

5. Uwasilishaji wa muziki, kisanii na maigizo ambayo yana mandhari ya kidini yanaweza kujumuishwa kwenye kazi za shule na programu kwa msingi wa kisanii na thamani ya elimu au matumizi ya kawaida ya kiulimwengu

5.1. Muziki, kisanii na maagizo maudhui yatatolewa kwa usawa, na siyo ya ibada kulingana na malengo ya programu ya ufundishaji, na kuambatana kwa kulinganisha kazi za wasanii wengine ambao siyo wa kidini.

5.1.1. Uwasilishaji wa muziki, kisanii na maagizo unaweza kufanywa kupitia ufanyaji wa kwenye mazingira maalumu yaliyoandaliwa, kama vile ukumbi wa maonyesho au chumba cha kwaya. Wakati unatafuta mahali pakufanyia muziki, sanaa na maonyesho wafanyakazi lazima kufuata vigezo vilivyoelezea kwenye INS-P033

5.1.2. Kama kuimba, sanaa au maigizo yanaendana na mambo ya kiroho, mfanyakazi lazima auwambie uongozi na kuwajulisha wanafunzi na wazazi ya kuwa ushiriki wa uwasilishaji ni uchaguzi. Wanafunzi hawataadhibiwa kwa kutoshiriki.

6. Kujifunza kazi maalumu kwenye sikukuu ambazo zinajumuisha dini na mambo ya ulimwengu kwenye vipengele vya sherehe (mfano, Krismasi) wanaweza kutambua dini kwenye kipengele na siyo kutambua kwenye ibada na ilimradi mwanafunzi hatatakiwa kufichua, kuchambua au kukosoa imani ya dini yao, kujumuisha isiyo kuwa na imani.

6.1. Wanafunzi binafsi wanaruhusiwa, kwa mwelekeo wao wenyewe, kutumia watu wa dini, matukio au alama kama magari ya kujielezea kisanii, na kama, inafaa na kulingana.na kazi waliyopangiwa.

7. Mfanyakazi hatarusiwa kushiriki kwenye shughuli zifuatazo kulingana na kujifunza kwa mwanafunzi:

7.1. Kutakiwa mwanafunzi kufichua, kuchambua au kukosoa imani ya dini yao kujumuisha kutokuwa na imani:

7.2. Kusahihisha kazi kwa kuelezea dini, kama ipo:

7.3. Kudhibiti au kuweka matokeo kwa wanafunzi ambao wanaelezea dini kulingana na sheria; au,

7.4. Kudhibiti imani ya kidini au kutokuwepo kwa imani ya kidini, kwa mfanyakazi juu ya mwanafunzi

8. Mwanafunzi anaweza kukataa kushiriki kwenye shughuli za shule zisizo na mafundisho ambayo ni kinyume na imani za kidini kiapo cha Utii; hata hivyo siyo tarajio kwamba wanafunzi wataepuka kwa kufishwa kwenye kuonyeshwa mawazo ambayo yanaingiliana na imani ya dini zao. Bila kuepukika, wanafunzi watasoma fasihi, kujifunza kuhusu dhana na kuchanganyika na watu wa lika lao wenye mfumo wa imani tofauti.

8.1. Wazazi, walezi na watoa huduma wenye haki ya kwenye elimu wanaweza kuchagua wanafunzi wao kutoshiriki shughuli za shule ambazo zinaingiliana na imani za kidini kufuatia vigezo vilivyoonyesha kwenye OAR 581.021.0009 na QAM CUR-P007

Sherehe na Mapambo Shuleni

9. Sherehe na mapambo shuleni lazima kuwa niya asili ya kiliumwengu na siyo kukuza dini maalumu

9.1. Pitia RSK-W008 kwa mwongozo kuhusu mapambo wakati wa sikukuu kwenye mazingira ya wilaya.

9.2. Kizuizi hakimkatazi mwanafunzi binafsi, kwa mtazamo wao wakionyesha mavazi yao ya sherehe za kidini, kuongea, kuandika au kuonyesha kwa namna nyingine.

Maombi

10. Kama suala la uhuru wa mtu binafsi mwanafunzi anaweza kujihusisha kwa hiari yake binafsi maombi yasiyo ya usumbufu wakati wowote yasiyoingiliana na masomo

10.1. Mfanyakazi wa shule usimtie moyo wala usimkatishe tamaa mwanafunzi kwenye kushiriki maombi yasiyo ya usumbufu au maombi ya kimya au shughuli yeyote ya ibada

Sheria ya Ufikiwaji Sawa ya 1984

11. Na kama kundi la wanafunzi lisolokuwa la mtaala wanaruhusiwa kukutana kwenye mazingira ya shule mara tu kabla au baada ya muda wa shule, wanafunzi wataruhusiwa kukutana na kuongelea dini, siasa, masuala ya kifalsafa au mengine, ili mradi mikutano hiyo ya kikundi, imeanzishwa, na inasimamiwa na wanafunzi

12. . Makundi ya kidini wanaweza kukodisha maeneo ya shule chini ya sera inayotoa huduma za kukodisha (FAC-P011). Shughuli za makundi kama hayo lazima kuonyesha utofauti kwenye shughuli zinazodhaminiwa na shule ili wilaya ya shule isiunge mkono au kuonekana kuunga mkono uanzishwaji wa dini

Nembo ya Dini

13. Mwanafunzi anaweza kuvaa vazi la dini au nembo ili mradi hazivurugi kwa kiasi kikubwa mchakato wa elimu kama ilivyoainishwa katika sera ya INS-A025

Udhuru kwa Sababu za Kidini

14. Pale ambapo mzazi, mlezi au mtoa huduma na anahaki ya elimu ataomba, mwanafunzi anaweza kusamehewa kushiriki kwenye sehemu ya mafunzo ya kidini kwa siku ya shule au wiki ya shule, ili mradi shughuli hazifanyiki kwenye maeneo ya shule. Kwa mujibu wa ORS 339.420, mwanafunzi wa shule ya msingi anaweza kusamehewa mpaka masaa 2 kwa wiki na wanafunzi wa sekondari wanaweza kusamehewa mpaka masaa 5 kwa wiki.

14.1. Alama za ufaulu hazitatolewa katika mafundisho hayo.

14.2. Mwanafunzi katika ngazi ya sekondari anaweza kuruhusiwa kutoka kipindi kimoja au zaidi ili kushiriki mafunzo ya dini pale ambapo mzazi, mlezi au mtoa huduma mwenye haki ya elimu ataomba. Shule katika hiki kipindi zitaandika hayupo kama ALIYERUHUSIWA kwenye Synergy na hawata andika vinginevyo

15. Pale ambapo maombi yatapokelewa kutoka kwa mzazi, mlezi au mtoa huduma mwenye haki ya elimu, mwanafunzi ataruhusiwa kutohudhuria shule ili kuadhimisha sikukuu ya kidini.

15.1. Mwanafunzi ambaye amerusiwa kutoka darasani au shule kwa ajili ya mambo ya kidini lazima wapewe fursa ya kufanya kazi walizopangiwa darasani na nyumbani au kukosa jaribio, kwa vile walikuwa hawapo.

Udhuru kwa Sababu ya Mila

16. Pale ambapo mzazi, mlezi au mtoa huduma na mwenye haki ya elimu ataomba mwanafunzi kuweza kusamehewa kushiriki kwenye kuadhimisha mila kwa sehemu ya shule au wiki ya shule, ili mradi shughuli hazifanyiki kwenye maeneo ya shule

16.1. Alama za ufaulu hazitatolewa katika mafundisho hayo.

17. Pale ambapo maombi yatapokelewa kutoka kwa mzazi, mlezi au mtoa huduma mwenye haki ya elimu, mwanafunzi ataruhusiwa kutohudhuria shule ili kuadhimisha sikukuu ya kiutamaduni

17.1. Mwanafunzi ambaye ameruhusiwa kutoka darasani au shule kwa ajili ya mambo ya kiutamaduni lazima wapewe fursa ya kufanya kazi walizopangiwa darasani na nyumbani au kukosa jaribio kwa vile walikuwa hawapo.

Kupanda darasa, Mahafali & Taratibu ya Kusherehekea

18. Hakuta kuwa na udhamini wa shule kwenye taratibu za kusherehekea. Wale wazazi wanaopenda walezi, watoa huduma na wanafunzi wanaweza kupanga na kusimamia taratibu za kusheherekea, ukizingatia kwamba huduma haitangazwi kupitia shule na ushiriki wa wafanyakazi na wanafunzi ni wa hiari.

19. Kupanda darasa na mahafali kunatakiwa kuwa huru bila ushawishi wa madhehebu pamoja na maombi na baraka

19.1. Matukio maalumu ya kiutamaduni ambapo maombi yanaambatana na tukio yamesamehewa

19.2. Shule au programu lazima kufanya juhudi zinafaa kuwataarifu wanafunzi na mgeni msemaji kabla ya tukio ili kuhakikisha kuwa mada, maudhui au madhumuni yanaendana na sera za wilaya.

Usambazaji wa Fasihi za Kidini

20. Mwanafunzi anaweza kusambaza fasihi za kidini chini ya hali sawa na fasihi nyingine ambazo zinaweza kusambazwa kwenye mazingira ya shule, ili mradi usambazaji huo hauingilii uendeshaji wa shule

20.1. Vifaa na/au matangazo kutangaza dini hayatasambazwa na mtu asiye mwanafunzi au kwa niaba ya vikundi au mtu binafsi asiye mwanafunzi

Huduma ya Kidini

21. Huduma za kidini, programu au mikusanyiko haitafanyika kwenye mazingira ya shule wakati wa muda wa masomo au kwenye shughuli zozote zinazohusiana na shule au shughuli zilizodhaminiwa na shule
22. Msemaji na/programu zinazozungumzia dini au ujumbe wa ibada haviruhusiwi

    22.1. Kizuizi hiki hakizuii uwasilishaji wa makusanyiko ya kwaya au muziki wa kidini au fasihi kama sehemu ya programu au mkusanyikio kama unavyoainishwa katika sehemu ya maagizo ya sera hii.

Malalamiko

23. Wanafunzi, wazazi, walezi, watoa huduma na wafanyakazi ambao wamechukizwa na vitendo au shughuli zinazofanywa katika shule au wilaya wanaweza kutoa wasiwasi wao kwa msimamizi wa shule kama ilivyoanishwa katika sera ADM-P008

Utaratibu wa Utekelezaji:

CUR-P007- Msamaha wa Kidini Kuchagua Kujiondoa

Historia ya Marekebisho:

Tarehe	**Maelezo**
10/07/22	**Sera Mpya**

Imepitishwa Na: Mkurugenzi wa Mipango ya Kimkakati